


Mwongozo wa Jamii wa Mkakati wa Mfuko wa Kimataifa Kuhusiana na Utambulisho wa Mapenzi na Jinsia (Sexual Orientation and Gender Identities)



KABLA HATUJAANZA, TUJIKUMBUSHE KUWA MFUKO WA KIMATAIFA UNAJIZATITIT KATIKA:

Kusaidia juhudi za afya ya umma ambazo zinashughulikia ukosefu wa usawa katika jamii na kijinsia, pamoja na tabia ambazo zinachochea ueneaji wa magonjwa haya matatu, ikizingatia elimu ya afya.



Kumaliza unyanyapaa na ubaguzi kwa wale walioathirika na kuambukizwa na Ukimwi, hususan kwa wanawake, watoto na watu walio katika hatari kubwa zaidi.

Kama njia ya kuondoa athari miongoni mwa watu walioathirika zaidi, Mfuko wa Kimataifa ulibuni Mkakati wa Jinsia. Unahusisha Mkakati wa Usawa wa Jinsia na Mkakati wa Utambulisho wa Mapenzi na Jinsia (SOGI). Hapa tunaangalia na Mkakati wa SOGI.

UTAMBULISHO WA MAPENZI NA JINSIA (SOGI) NI NINI?

Uwezo wa kila mtu waa hisia, mapenzi na kivutio cha penzi, pamoja na mahusiano ya kimapenzi na watu wengine (iwe kwa jinsia moja ama zaidi)

Kila hisia ya ndani ya mtu minghairi ya jinsia, ambayo inaweza kuwa ya jinsia moja kama ilivyokuwa wakati wa kizaliwa, pamoja na hisia binafsi za mwili na kujieleza kwingine katika jinsia, ikiwa ni pamoja na mavazi, lugha na tabia.



Lengo katika Utambulisho wa Mapenzi na Jinsia ni juu ya watu wote ambao mwelekeo wao wa kimapenzi, utambulisho wa kimapenzi na/ama tabia za kimapenzi haziendani na tabia na maadili ya wengi, ikilenga watu wazima wanaojihusisha na mapenzi kwa maamuzi yao ambayo inaongeza athari katika afya zao.

WATU WENYE UTAMBUZI MBADALA WA MAPENZI (SEXUAL MINORITIES) NI AKINA NANI?

Watu hawa wana mazoea tofauti na athari tofauti za kiafya. Wanapata changamoto katika kupata ama kufaidi misaada ya Mfuko wa Kimataifa na wanapata vizuizi vya kijamii na kimfumo katika kupata afya na haki. Katika muktadha mara nyingi wanakumbwa na unyanyapaa na ubaguzi kulingana na utambulisho wao wa mapenzi, huduma za kuzuia maambukizo zimekumbwa na changamoto na sheria za kuzuia ushoga zimepelekea kunyimwa kwa huduma za kiafya.



BAADHI YA MAMBO YA UKWELI:

- Ukimwi bila kujali pia inaathiri watu wenye utambuzi mbadala wa mapenzi
- Ueneaji wa Ukimwi miongoni mwa wauza ngono ni juu kukiko watu wa kawaida
- Ueneaji wa Ukimwi miongoni mwa wanaume wnaofanya mapenzi na wanaume wenzao ni juu (asilimia **25%** Afrika, asilimia **11%** Caribbean, asilimia **28%** Asia Kusini Mashariki na juu kama asilimia **51%** sehemu za Amerika Kusini).
- Hata idadi kubwa zaidi za ueneaji zipo miongoni mwa watu waliobadilisha jinsia (transgender).

• **ILI KUFIKIA MAHITAJI YA JAMII YA SOGI, MFUKO WA KIMATAIFA UNALENGA MAMBO MAKUU YAFUATAYO. MENGINE YANELEZWA HAPA KWA MUHTASARI:**

MALENGO	HII INAMAANISHA NINI?	JE UMUHIMU WAKE KWETU?
1. Kuimarisha Mifumo ya Kiuratibu ya Nchi	1. Kutoa mwelekeo ili kuimarisha utaalamu na uwezo kuhusiana na SOGI	Mfuko wa Kimataifa unataka kuhakikisha kwamba (hususan ikifika suala la SOGI) kwamba ujuzi katika ngazi ya chini na uzoefu uneongozwa Katika muktadha wa mipango ya SOGI unatengwa, Mfuko wa Kimataifa unatoa maombi ya ufadhili fursa nje ya Mifumo ya Kiuratibu ya Nchi (CCM).
2. Kuipitia tena Miongozo ya Maombi ya Misaada	2. Kuhakikisha uwezo na utaalamu kuhusiana na SOGI ni sehemu ya maombi ya misaada	
3. Kushirikiana na Washirika wa Mfuko wa Kimataifa	3. Kuelekea mbele, masuala ya jinsia na athari zitakuwa sehemu ya ushirikiano. Kutakua na msaada katika kuimarisha jamii	
4. Uenezi na Masiliano	4. Kufuatilia na kuhabarisha uvunjaji wa haki za binadamu na sheria za kupinga ushoga kuhusiana na SOGI	



WASILIANA NA MPANGO WA KIKANDA

Regional Platform for Communication and Coordination for Anglophone Africa Hosted by
EANNASO Arusha, Tanzania Tel: +255 737 210598 Email: eannaso@eannaso.org | Website:
www.eannaso.org

Facebook: www.facebook.com/eannaso.org | Twitter: [@eannaso](https://twitter.com/eannaso)